

TAARIFA YA WILAYA YA MUSOMA KWA MKUU WA MKOA WA MARA MHE. CAPT. ASERI MSANGI

1.0. MAELEZO MAFUPI YA HALMASHAURI YA MANISPAA YA MUSOMA:

1.1 Utawala

Mhe. Mkuu wa Mkoa,

Eneo la Wilaya ya Musoma ambalo pia ndio eneo la Manispaa ya Musoma kuna Tarafa 1 ya Musoma Mjini. Zipo kata 16 ambazo ni Mukendo, Mwigobero, Kitaji, Iringo, Nyasho, Kamunyonge, Mwisenge, Makoko, Buhare, Nyamatare, Kigera, Kwangwa, Nyakato, Mshikamano, Rwamlimi na Bweri. Kata zote 16 zina jumla ya Mitaa 73.

1.2. Siasa

Wilaya ya Musoma ina Jimbo moja la Uchaguzi ambalo ni Musoma Mjini. Kutokana na Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2010, Chama cha Mapinduzi kilipata viti 3 vya udiwani na Vyama vya Upinzani kwa ujumla wake vilipata viti 10 vya Udiwani. Hivyo CCM ina Madiwani 4, CUF 3 na CHADEMA 11 na kiti cha Ubunge kilichukuliwa na CHADEMA

Katika Uchaguzi wa viongozi wa mamlaka ya Serikali za mitaa uliofanyika tarehe 14/12/2014, Mitaa yote 73 na Kata zote 16 zilishiriki uchaguzi huo.

Chama cha Mapinduzi kilipata viti vya Wenyeviti wa Mitaa **42** na chama cha Demokrasia na Maendeleo kilipata viti **29** katika uchaguzi huo mitaa miwili (**2**) ya Zanzibar (Makoko) na Kitaji D (Kitaji) matokeo ya uchaguzi hayakutolewa baada ya kutokea vurugu na fujo ambazo zingepolekeleka kuhatarisha usalama wa wasimamizi wa uchaguzi, askari wa vituo na wananchi kwa ujumla. Marudio ya uchaguzi katika mitaa hiyo ulikuwa umepangwa kufanyika tarehe **21/12/2014** lakini ulisitishwa kwa amri ya Mahakama mpaka shauri lililowasilishwa Mahakamani litakapotolewa ufumbuzi.

2.0. HALI YA UTUMISHI

Mhe. Mkuu wa Mkoa,

Kwa mujibu wa ikama iliyoidhishwa mwaka wa fedha 2014/2015 ambayo ndiyo tumeendelea kutekeleza kwa mwaka wa fedha 2014/2015. Halmashauri ina mahitaji ya watumishi **2,110**, hadi kufikia tarehe **31 Mei 2015**, Halmashauri ilikuwa na jumla ya watumishi wapatao **1,665**, hivyo kutokana na uhalisia wa mahitaji hayo kunaifanya Halmashauri ya Manispaa ya Musoma kuwa na upungufu wa watumishi **445**.

3.0. UTEKELEZAJI WA ILANI YA UCHAGUZI YA CCM (2010-2015)

Mhe. Mkuu wa Mkoa,

Halmashauri ya Manispaa ya Musoma inaendelea kutekeleza ilani ya uchaguzi ya CCM (2010-2015) kama ilivyoanishwa kwenye ibara mbalimbali kama vile

Mapinduzi ya Kilimo kutekelezwa kwa ukamilifu, malengo ya mpango wa maendeleo ya Sekta ya Kilimo na Kauli mbiu ya Kilimo kwanza (Ibara ya 33)) ambapo ushauri kuhusu kanuni bora za kilimo umetolewa kwa wakulima **5,430** na pia elimu imetolewa kwa wakulima kupitia **vikundi 12** vya wakulima , Vikundi 3 vimewezeshwa kuanzisha kilimo cha mazao ya bustani kwa kutumia teknolojia ya Vyama 9 vya ushirika vimeanzishwa.Nyumba, Mipango Miji, Upimaji na ramani (Ibara ya 60) ambapo michoro ya kimipango miji 9 imeandaliwa na jumla ya viwanja **1,268** vilipimwa. Aidha Halmasahuri ilitoa eneo kwa ajili ya ujenzi wa nyumba za makazi katika Kata ya Buhare.

Ajira (Ibara ya 22) ambapo tatizo la upungufu wa ajira limeendelea kushughulikiwa na Wilaya pamoja na wadau wake wa maendeleo. Juhudi zimefanyika kuhamasisha jamii ili kuanzisha vyama vya ushirika ambapo Halmashauri katika mapato yake imechangia **Tshs. 60,000,000.00** kwa ajili ya mikopo ya vikundi vya wanawake na vijana. Vikundi vya vijana 37 na 70 vya wanawake wamenufaika na mfuko huo. Changamoto zilizojitokeza wakati wa utoaji wa mikopo ni pamoja wakopaji wengi ni wanawake na mikopo inayotolewa hupokonywa na baadhi ya wanaume, upungufu wa elimu ya ujasiriamali kwa wanavikundi na mahitaji ya wakopaji kuwa juu kuliko uwezo wa wakopeshaji.

4.0. BARABARA:

Mhe. Mkuu wa Mkoa,

Wilayaya Musoma ina jumla ya kilomita 416.58 za mtandao wa barabara kwa mgawanyo ufuatao:-

- Barabara za Lami Kilomita 7.60
- Barabara za Changarawe Kilomita 312.17
- Barabara za Udongo Kilomita 96.81

Halmashauri ya Manispaa ya Musoma ni miongoni mwa Halmashauri za Manispaa na Miji kumi na nane (18) nchini ambazo ziliteuliwa na Serikali kwa ajili ya kuboresha miundombinu mjini kwa kutumia fedha za mkopo wa Benki ya Dunia. Katika Programu hii ambayo imepangwa kwa miaka mitano (**5**) kuanzia mwaka **2013/2014** hadi mwaka **2017/2018**, Halmashauri ya Manispaa ya Musoma imetengewa jumla ya Dola za Kimarekani **9,585,615.68** sawa na Tshs. **15,336,985,088.00**.

Kwa mwaka wa fedha **2014/2015** Halmasahuri ya Manispaa ya Musoma imetengewa jumla ya Shs **2,606,435,200.00** kutoka Benki ya Dunia ambapo shughuli zifuatazo zimepangwa kufanyika.

- Kusanifu kwa kiwango cha lami barabara zenye urefu wa kilomita **10.15 (Mutex – Buhare, Kennedy, Karume, Amri Abeid, Makongoro, Maktaba, Serengeti, Uhuru, Lumumba, Kusaga, Rutigingi, Gandhi na Nyasho sokoni – nyasho Majita)**
- Kusanifu soko la Nyasho
- Ujenzi wa barabara ya Nyasho – Majita

5.0. HUDUMA ZA JAMII:

5.1. ELIMU YA MSINGI:

Mhe. Mkuu wa Mkoa;

Hali ya utoaji wa Elimu katika wilaya yetu ni nzuri ambapo Wilaya imejitahidi kwa kushirikiana na wananchi kujenga shule za msingi. Wilaya inazo jumla ya Shule za Msingi **46** ambapo za Serikali ni **38** na binafsi ni **08**.

5.2.0. ELIMU YA SEKONDARI:

Mhe. Mkuu wa Mkoa,

Halmashauri ya Manispaa ya Musoma ina jumla ya shule za Sekondari **25** zenye jumla ya wanafunzi **11,915** kati ya hao **7,059** ni wavulana na **4,856** ni wasichana. Shule **18** zinamilikiwa na Serikali na shule **7** siyo za Serikali. Miongoni mwa shule za Sekondari za Serikali Shule **3** zina kidato cha **V** na **VI** na ni za bwani na shule **15** zina kidato cha **I** hadi kidato cha **IV** na ni za kutwa.

5.2.1. MPANGO MKAKATI WA UJENZI WA MAABARA

Mhe. Mkuu wa Mkoa,

Ujenzi wa maabara katika Halmashauri ya Musoma unatekelezwa kwa kuzingatia agizo la Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania la kila shule kuwa na maabara tatu za sayansi. Utekelezaji wa agizo hilo ulianza kwa ushirikiano kati ya viongozi wa Wilaya ya Musoma, viongozi wa Halmashauri ya Manispaa ya Musoma na Wadau mbalimbali wa maendeleo katika Halmashauri ya Manispaa ya Musoma.

Mhe. Mkuu wa Mkoa,

Kwa mujibu wa taarifa hiyo jumla ya vyumba vya maabara **46** vilitakiwa kujengwa na gharama ya kila maabara moja pamoja na vifaa vyake ilikadiriwa kuwa shilingi **milioni 75** sawa na shilling **3,450,000,000.00** kwa maabara **46**. Halmashauri ya Manispaa ya Musoma kwenye bajeti ya mwaka 2014/2015 ilipanga kutumia shilingi **409,775,000.00** na kiasi hiki kilipatikana baada ya kubadili matumizi ya vifungu vingine vya miradi ya maendeleo vilivyokuwa vimetengewa fedha kwenye Bajeti yake ya mwaka 2014/2015 ambapo shilingi **47,000,000.00** ilikusudiwa zitokane na mapato ya ndani na shilingi **362,775,000.00** ruzuku kutoka Serikali kuu.

Mhe. Mkuu wa Mkoa,

Halmashauri inakabiliwa na changamoto zifuatazo katika ujenzi wa maabara:-

- Baadhi ya wanasisia kupinga uchangiaji wa ujenzi wa maabara kwa kauli wanazozitoa wakiwa kwenye mikutano yao ya siasa. Kauli hizi zimesababisha baadhi ya wadau na wananchi waliokuwa na nia ya kuchangia ujenzi wa maabara wasite na wengine kuacha kabisa kutoa michango.

- Fedha zilizotengwa na Halmashauri kwa ajili ya ujenzi wa maabara hazijapatikana zote kutokana na Serikali Kuu kutotoa fedha za maendeleo kwa wakati.
- Wananchi na baadhi ya makampuni yaliyotoa ahadi ya vifaa na fedha kwa ajili ya ujenzi wa maabara hawajakamilisha ahadi zao licha ya kufuatiliwa mara kwa mara.

5.2.2.MIKAKATI YA KUKAMILISHA UJENZI WA MAABARA

Halmashauri ya Manispaa ya Musoma imejiwekea mikakati ifuatayo kwa ajili ya kuiwezesha kukamilisha ujenzi wa maabara:-

- Kuendelea kuhimiza michango ya ujenzi wa maabara kutoka wadau mbalimbali.
- Kufuatilia fedha za miradi toka Serikali Kuu ili ziweze kutumika kwenye ujenzi wa maabara.
- Kuendelea kutoa Elimu ya umuhimu wa maabara za Sayansi kwa jamii ya wakazi wa Halmashauri ya Manispaa ya Musoma, na Taifa kwa ujumla.

6.0.HUDUMA ZA AFYA:

6.1. VITUO VYA KUTOLEA HUDUMA ZA AFYA

Mhe.Mkuu wa Mkoa, Halmashauri ya Manispaa ya Musoma ina jumla ya vituo 26 vya kutolea huduma za afya.

Aidha Halmashauri ina jumla ya maduka ya dawa muhimu 80 na Famasi 5 na tunategemea kufungua Zahanati ya Nyamatare ambayo ujenzi wake upo kwenye hatua za mwisho.

7.0. HALI YA UTENDAJI KAZI KWA KIPINDI CHA MWAKA 2014

7.1. WAGONJWA WALIOHUDUMIWA

Mhe.Mkuu wa Mkoa, Katika kipindi cha mwaka 2014, jumla ya wagonjwa **137,139** kama wagonjwa wa nje waliweza kupatiwa huduma za afya katika vituo vyetu. Kati ya hao wanawake walikuwa **82,234** na wanaume walikuwa **54,905**. Kwa upande wa wagonjwa wa waliolazwa jumla ya wagonjwa **9,522** walilazwa, kati ya hao wanaume walikuwa **3,808** na wanawake walikuwa **5,714**.

8.0. UTEKELEZAJI WA MKAKATI WA MKOA WA KUPUNGUZA VIFO VYA AKINA MAMA WAJAWAZITO NA WATOTO WACHANGA

Mhe.Mkuu wa Mkoa, Halmashauri ya Manispaa ya Musoma ilianza kutekeleza Mkakati wa Mkoa wa kupunguza vifo vya akina mama wajawazito na watoto wachanga tangu Julai 2013. Kwa mujibu wa mkakati huo, lengo la Halmashauri ya Manispaa ya Musoma ilikuwa ni kupunguza vifo vya akina mama kutoka 20 mwaka 2012 hadi 10 ifikiapo mwaka 2016. Katika lengo kuu hilo kuna malengo mahsusi (**specific objectives**) sita (6) yafuatayo;

1. Kuboresha vituo vya afya ili viweze kutoa huduma ya kujifungua kwa njia ya kupasuliwa na kuongeza damu salama.
2. Kusajili wanawake wote wajawazito na kuwafuatilia ili waende kliniki na kujifungulia katika vituo vya kutolea huduma.
3. Kuwahimiza akina mama wajawazito baada ya kujifungua wajiunge na uzazi wa mpango.
4. Kuboresha mfumo wa rufaa za wagonjwa.
5. Kuongeza idadi ya watumishi wa kada ya Afya.
6. Kuboresha vikao vya ngazi ya kata na mitaa kwa ajili ya kujadili taarifa za utekelezaji.

Mhe.Mkuu wa Mkoa, Tangu Julai 2013, Manispaa ya Musoma imefanya yafuatayo katika kutekeleza malengo mahsusi yaliyotajwa hapo juu:

- I. Vifo vimepungua kutoka 20 mwaka 2012/2013 mpaka 14 kwa kipindi cha Julai, 2014 - Mei, 2015. Vifo hivi vyote hutokea katika Hospitali ya Mkoa, na nusu ya vifo hivyo si vya wakazi wa Manispaa ya Musoma. Vyanzo vikuu vya vifo hivyo ni kuchelewa kufikishwa Hospitalini na upungufu wa damu.
- II. Vikao viwili vimefanyika kwa maafisa watendaji wa kata 13 na wa mitaa 57 kwa kutoa maelekezo mbalimbali kwa ajili ya utekelezaji wa mkakati huu.
- III. Motisha ya Tsh.10, 000/= inatolewa kwa waganga na wauguzi wanaozalisha vituoni ili kuongeza kiwango cha uzalishaji.
- IV. Akina mama waliojifungua wanaendelea kufuatiliwa baada ya saa 24, siku 7, siku 28 na siku 42 ili kujiridhisha na afya ya mama na mtoto wake.
- V. Katika kipindi hicho, Jumla ya watumishi wa afya 34 wa kada mbalimbali wameajiriwa na wote wapo kazini mpaka sasa na mkakati wa kuwatunza upo. Pia watumishi 11 wamepelekwa katika vyuo mbalimbali vya afya ili kuongeza ujuzi wao.
- VI. Mfumo wa rufaa umeboreshwa kwa kuwa na magari ya wagonjwa (ambulance) mawili ambayo yanatoa huduma muda wote (saa24) katika vituo vyote vilivyopo katika manispaa yetu.
- VII. Kituo cha Afya Nyasho kimeboreshwa kwa kukarabati vyoo vya wagonjwa wa nje matundu 6, kununua vitanda vya kuzalishia na vya wagonjwa wa kawaida, kununua vyandarua na mashuka, kuongeza upatikanaji wa dawa ikiwa ni pamoja

na kuimarisha stoo ya madawa. Nyumba ya upasuaji pamoja na vifaa vyake viko tayari inasubiri kufunguliwa.

9.0. TAARIFA YA MFUKO WA AFYA YA JAMII (CHF)

Mhe.Mkuu wa Mkoa, Mfuko wa afya ya jamii, katika Halmashauri ya Manispaa ya Musoma kwa sasa uma jumla ya kaya **810 (11.8%)**, hii ni kwa mujibu wa takwimu za hadi mwezi Machi 2015.

10.0. MAPATO YA NDANI

Mhe. Mkuu wa Mkoa,

Mapato ya ndani yamekuwa yakiongezeka baada ya Halmashauri kuchukua hatua mbalimbali katika kuimarisha ukusanyaji wa mapato yake ya ndani. Hatua hizo ni pamoja na:-

- Kutoa matangazo sehemu mbalimbali kuhamasisha wafanya biashara kulipa ada za leseni kwa mujibu wa sheria.
- Kuunda timu ya ufuatiliaji mapato kwa kila chanzo.
- Kuhakikisha kuwa wafanyabiashara wote wanaofanya biashara na Halmashauri wanalipa ushuru wa huduma kila malipo yanapofanyika na ufuatiliaji kwa wafanyabishara wengine kwa mujibu wa sheria unafanyika
- Kuimarisha takwimu za walipa kodi ili kuziba mianya ya wakwepa kodi
- Wadau mbalimbali wakiwemo viongozi na watendaji wa Halmashauri kuendelea kutoa elimu kwa walipa kodi.

10.1. UTATUZI WA KERO MBALIMBALI ZA WANANCHI

Mhe. Mkuu wa Wilaya,

Halmashauri ya Manispaa ya Musoma inalo dawati la malalamiko linaloshughulikia kero mbalimbali za wananchi. Dawati la malalamiko limeanzishwa katika ngazi zote za utawala kwa maana ya Mitaa na Kata.

Mhe. Mkuu wa Mkoa,

Kwa heshima na taadhima naomba kuwasilisha.

Dr.Khalfany Haule
**MKURUGENZI WA MANISPAA
HALMASHAURI YA MANISPAA
MUSOMA**